**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI**

**021** **KISWAHILI**

**Muda: 2:30** **MAJIBU** **Mwaka: 2016**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii in sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi (10)** .

2. Jibu maswali **yote** .

3. Majibu **yote** yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.

4. Majibu yote yaandikwe kwa kaalamu yenye wino wa bluu au mweusi.

5. Vifaa **vyote** vya mawasiliano visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.

6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org
*Prepared by Maria Marco for TETEA*

## UFAHAMU

1. Soma hadithi ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata:

Katika nchi ya ughaibuni kulikuwa na mfalme mwenye dharau na maringo sana, aliwaona wananchi wake kama wajinga. Watu wake waliishi bila amani na walichukia vitendo vya mfalme wao. Mfalme huyo alikuwa anajigamba kuwa yeye ni tajiri kuliko wafalme wote katika nchi za jirani. Kwa ujumla mfalme huyo alikuwa mnyanyasaji na mwenye kebehi nyingi.

Mfalme alikuwa mwenye kufuru sana, hata alidiriki kutamka kwenye mkutano wa hadhara kuwa hajawahi kuona njaa. Mzee mmoja mwenye busara aitwaye Bwana Adili alimwambia mfalme kuwa asihofu atampeleka mahali njaa inakopatikana. Bwana Adili kwa kukubaliana na mfalme walipanga siku ya safari ya kwenda kumwonesha mahali ilipo njaa. Safari hiyo ilikuwa na masharti kuwa hakuna kula chochote asubuhi na hakuna kubeba masurufu yoyote yakiwemo maji, ingawa Bwana Adili kwa ujanja wake alibeba.

Safari ilianza asubuhi mapema huku mfalme akiwa na furaha kubwa ya kwenda kuona njaa. Walitembea mwendo wa saa zisizopungua sita, mfalme akawa amechoka sana akamwomba Bwana Adili wapumzike. Uchovu huo ulitokana na ukweli kwamba mfalme hakuwahi kwenda mwendo mrefu kwa miguu. Wakati wa mapumziko mfalme alimwomba Bwana Adili maji na mkate lakini Bwana Adili alimnyima, walipumzika kwa muda wa saa moja na safari ikaendelea. Ilipofika jioni mfalme alikuwa amechoka kabisa kwani mwendo ulikuwa mrefu na njaa ilimuuma mno. Walipumzika chini ya mti, mfalme alimuuliza Bwana Adili, mbona hatufiki safari yetu? Bwana Adili hakumjibu chochote bali alichukua mkate akala na kunywa maji, mfalme alihisi njaa kali, alimwomba Bwana Adili mkate na maji lakini alimnyima.

Hali ya mfalme ilizidi kuwa mbaya sana, ndipo Bwana Adili akamwambia nitakupa maji na mkate ule lakini uahidi kwa maandishi kuwa utaacha dharau na majivuno kwa watu. Mfalme alipiga magoti mbele ya Bwana Adili na kuchukua karatasi na kalamu aliyopewa na Bwana Adili na kuahidi kwa maandishi kuwa ataacha kabisa tabia ya dharau na majivuno. Bwana Adili alipokea maelezo ya mfalme na akampa mkate na maji. Mfalme alipomaliza kula alimshukuru sana, ndipo Bwana Adili alipomgeukia mfalme na kumweleza kuwa hakuna maskani ya njaa bali hali aliyokuwa nayo ya kuhitaji chakula ndiyo njaa, ni kitu ambacho hakionekani ila ni hali apatayo mtu asipokula chakula. Waliporudi mfalme alitisha mkutano wa hadhara, aliwaomba radhi wananchi wake na tangu siku hiyo mfalme aliishi kwa upendo na wananchi wote.

Maswali

(a) (i) Bwana Adili alitoa masharti gani ya safari?
(i) Hakuna kula chochote asubuhi.
(ii) Hakuna kubeba masurufu yoyote yakiwemo maji.
(ii)Kwa nini Bwana Adili alitoa masharti uliyoeleza katika kipengele (a)(i)?
Aliweka masharti hayo ili kumfundisha mfalme maana halisi ya njaa kupitia uzoefu wake binafsi.

(b) Toa methali moja inayolingana na fundisho linalopatikana katika hadithi uliyosoma.
Methali: Jambo usilolijua ni Kama usiku wa giza

(c) Toa maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika hadithi uliyosoma:


Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org
***Prepared by Maria Marco for TETEA***

(i) Anajigamba - Kujisifu
(ii) Kebehi - Dharau
(iii) Kufuru - Kutenda mambo yanayokiuka maadili
(iv) Masurufu - Vifaa au chakula cha kusafiria
(v) Maskani - Makazi au mahali pa kuishi

(d) Andika ufupisho wa habari uliyosoma kwa maneno 60.

**Kulikuwa na mfalme mwenye dharau aliyepelekwa safari na Bwana Adili ili ajifunze maana ya njaa. Baada ya kuhisi uchungu wa njaa, mfalme aliandika ahadi ya kubadilika na kuishi kwa upendo na watu wake.**

## SEHEMU B.
## MATUMIZI YA LUGHA NA USAHIHI WA MAANDISHI

2. (a) Andika kwa usahihi maneno yaliyokolezwa wino kama yalivyotumika katika tungo zifuatazo:
(i) **Mashirikiano** ni muhimu kwetu ...., Ushirikiano
(ii) Mimi ni **Mwanainji** wa tanzania...... Mwananchi
(iii) Mama **anakaaga** jikoni anapopika.... huwa amekaa
(iv) Hakuna **mapungufu** yaliyojitokeza..... Upungufu
(v) Hajafika mwanafunzi **yoyote** leo ........ Yeyote
(vi) Huyu ni rafiki **angu** .......... yangu

(b) Eleza maana mbili kwa kila tungo.
(i) Mama anaota.
- kitendo Cha kupata joto kupitia jua au moto.
- kitendo Cha kuona njozi mtu anapokuwa amelala

(ii) Nipe Sahani ya kulia
- Sahani iliyo mkono wa kuume.
- Sahani inayotumiwa kwa kula chakula.
- Sahani inayotoa mlio, yaani inayolia.

(iii)Vijakazi wanalima Barabara
- njia pana yanayopita magari.
- Barabara - vizuri; sawa sawa.

(iv)Amekanyaga mtoto
- Mtoto amefanya kitendo cha kukanyaga kitu ama mtu
- Mtu ama mnyama amefanya kitendo cha kuweka miguu yake juu ya mtoto

(v) Shangazi anawachezea wanangu
- Shangazi anacheza kwa ajili ya wanangu
- Shangazi anacheza kwa niaba ya wanangu

(c) Andika KWELI kama sentensi ni sahihi au SIO KWELI kama sentensi si sahihi.

(i) Tafadhari mpikie ugali. Hii ni tungo tata. KWELI
(ii) Kifaa kinachotumila kulia chakula kinachoiwa Uma wingi wake ni uma. SIO KWELI
(iii) Rejesta ni misimu ya Kiswahili. SIO KWELI
(iv) Amekula chumvi nyingi. Hii ni nahau. KWELI
(v) Mbili kutwa Mara tatu. Hii ni rejesta ya kujifuza hesabu. SIO KWELI

**SEHEMU C**
**SARUFI**

3. (a) Bainisha aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika tungo zifuatazo:
Mfano: sisi tunacheza mpira uwanjani.
jibu: kiwakilishi
(i)Kuku **yu** bandani -kiima
(ii)Maskini! Ameumia! - Kihisishi
(iii)Wako hatakiwi hapa - Kiwakilishi
(iv)Dagaa wa kigoma ni watamu - Nomino
(v)Mtoto alikuwa anacheza mpira - Kitenzi kisaidizi

(b) Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo:
(i) umba ........ **Kuumba**
(ii) Pigo - **Kupiga**
(iii) Mteule **Kuteua**
(iv)Mlinzi - **Kulinda**
(v) Kiongozi - **Kuongoza**
(vi) Mchezo - **Kucheza**
(vii)Adhabu - **Kuadhibu**
(viii) Muundo - **Kuunda**
(ix)Chakula- **Kula**
(x) Mtego- **Kutega**

(c) Tunga sentensi kwa kutumia aina za maneno zifuatazo:
(i) Mimi litumike kama kiwakilishi
Mimi nitashughulikia tatizo hilo.

(ii)Letu litumike kama kivumishi
Hili ni darasa letu.

(iii) Tutaendelea litumike kama kitenzi kisaidizi
Tutakuwa tayari kufanikisha mradi.

(iv)Na litumika kama kiunganishi
Baba na mama wameondoka.

(v)Upendo litumike kama nomino dhahania
Upendo huleta mshikamano.

## SEHEMU D
## FASIHI SIMULIZI

4. (a) Kamilisha methali zifuatazo:
(i) Kuishi kwingi ni **kuona mengi**.
(ii) Mchuma janga **hula na wa kwao.**
(iii) Chanda chema **huvikwa pete**.
(iv) Asiyekubali **kushindwa si mshindani.**
(v) Jambo usilolijua ni sawa **na usiku wa kiza**.

(b) Bainisha tofauti tano zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.
(i) Fasihi simulizi hupitishwa mdomo kwa mdomo; fasihi andishi huandikwa.
(ii) Fasihi simulizi huhitaji hadhira moja kwa moja; fasihi andishi inaweza kusomwa binafsi.
(iii) Fasihi simulizi huhifadhiwa kwenye kumbukumbu ya mdomo; fasihi andishi huhifadhiwa katika maandishi.
(iv) Fasihi simulizi hubadilika kulingana na mtoa hadithi; fasihi andishi huwa thabiti.
(v) Fasihi simulizi hutegemea sana matumizi ya sauti; fasihi andishi hutegemea maandishi.

(c) Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.

Mada iliyo moyoni, hii ninawaletea,
Watoto wa mitaani, mada nimeshafungua,
Wanapata mitihani, katika hii dunia,
Nawaonea huruma, imewatupa dunia.

Wanashinda jalalani, hayo ndiyo mazoea,
Umkute kituoni, anaomba abiria,
Ni njaa mwake tumboni, ndiyo inamsumbua,
Ataomba kwa imani, huku anakulilia.

Wapo pia maaluni, vibaya wamezoea,
Hawaombi wala nini, kazi yao kukwapua,
Husimama vituoni, abiria kuvizia,
Abiria wanalia, kila kitu kimekombwa.


Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org
***Prepared by Maria Marco for TETEA***

Twajenga taifa gani, watoto kuachilia?
Wazurure mitaani, na sisi twachekelea,
Tunadhania utani, na mwishowe tutalia,
Kwani mzaha mzaha, hutumbukia usaha.

(i) Bainisha Muundo na mtindo wa shairi.
- Muundo wa shairi hili:
Ni shairi la kikale, lenye beti nne na mistari minne kila ubeti.
- Mtindo wa shairi hili:
Mtindo wa kutumia taswira za huruma na maonyo.

(ii)Eleza dhamira ya mtunzi katika ubeti wa pili
- Dhamira ya mtunzi katika ubeti wa pili ni Kueleza mateso ya watoto wa mitaani wanaoishi kwa njaa na mahangaiko.

(iii)Eleza Ujumbe wa shairi hili.
- Tuwajali watoto wa mitaani na kuwapatia msaada ili kuondoa mateso yao.

(iv) Toa Methali nyingine yenye maana sawa na methali iliyopo katika beti wa nne.
Samaki mkunje angali mbichi.

(vi)Andika kichwa Cha habari Cha shairi hili kisichozidi maneno matano na kisichopungua maneno matatu.
Kichwa cha habari: **Watoto wa Mitaani**

**SEHEMU E.**

**UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI.**

5. Wewe ni mwanafunzi wa Kidato cha Pili katika Shule ya Sekondari Tegemeo, S.L.P 130, Dodoma. Una matatizo ya kiafya hivyo unahitaji kwenda kutibiwa hospitali ya Mkoa wa Dodoma. Andika barua kwa Mkuu wako wa Shule kuomba ruhusa ya siku mbili (02). Jina lako liwe Juhudi Sabuni.


Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org
***Prepared by Maria Marco for TETEA***

**Barua:**

Juhudi Sabuni,
Shule ya Sekondari Tegemeo,
S.L.P 130,
Dodoma.
21/12/2024.

Kwa: Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Tegemeo,
S.L.P 130,
Dodoma.

YAH: OMBI LA RUHUSA YA SIKU MBILI KWA MATIBABU

Ninayo heshima kuandika barua hii nikiomba ruhusa ya siku mbili (22-23/12/2024) kwa ajili ya kwenda hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu kutokana na matatizo ya kiafya.

Ninaahidi kurejea shuleni mara baada ya matibabu na kuendelea na masomo kama kawaida.

Naomba ruhusa yangu izingatiwe.

Wako mtiifu,
Juhudi Sabuni.



Find this and other free resources at http://maktaba.tetea.org
***Prepared by Maria Marco for TETEA***